

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KWANZA

05 APRILI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 05 APRILI, 2022

I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:

II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUWANZA SAA 3:00 ASUBUHI:

III. KIAPO CHA UAMINIFU:

Mhe. Shamsi Vuai Nahodha

IV. TAARIFA YA SPIKA:

V. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

VI. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

1. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Wananchi wa Ifakara watapewa fedha za ujenzi wa Soko la Halmashauri ya Mji wa Ifakara ambao umesuasua kwa muda sasa.

2. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Ivuna hadi Chole ili kurahisisha mawasiliano kati ya Wilaya ya Momba na Songwe.

3. MHESHIMIWA SIMON SONGE LUSENGEKILE (BUSEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-


Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha Kituo cha Afya Kiloleli pamoja na kupeleka Vifaa kwenye Hospitali ya Wilaya Busega.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):


4. MHESHIMIWA MWANTUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuingiza Wananchi wengi zaidi kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.



WIZARA YA KILIMO:



5. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itajenga miradi ya umwagiliaji katika Tarafa ya Malangali ili Wananchi waweze kushiriki katika kilimo cha umwagiliaji.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

6. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua magari mapya ya Polisi kwa ajili ya Vituo vya Polisi nchini.

7. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Polisi katika Tarafa za Kipatimu, Njinjo na Nanjilini Wilayani Kilwa.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

8. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kuu ya Mwanza - Shinyanga kwa kiwango cha njia nne kutoka Mwanza Mjini hadi Usagara.

9. MHESHIMIWA KILUMBE SHABAN NG'ENDA (KIGOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kuboresha usafiri wa reli wa Kigoma – Dar es Salaam ambao unafanya safari mbili kwa wiki.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

10. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango wa kutoa fidia kwa Wananchi wa Simiyu wanaopakana na Hifadhi za Wanyamapori na kuathiriwa na Wanyama hao.

**DODOMA
05 APRILI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**